BUSEGA DC JARIDA

Toleo Na. 4

APRILI, 2022

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSEGA

TOLEO LA ROBO YA TATU 2021/2022

Linatolewa Na Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Busega, S.L.P 157

www.busegadc.go.tz
@busegadc busegadc
@busegadistrict halmashauri ya wilaya ya busega

YALIYOMO

UTANGULIZI 1

Lengo la Jarida..... 1

Habari na Matukio Yaliyojiri Robo ya Kwanza 2021/2022.....2-16

UTANGULIZI

Halmashauri ya Wilaya ya Busega ni mojawapo ya Halmashauri 6 zilizopo Mkoa wa Simiyu. Halmashauri ya Wilaya ya Busega imeanzishwa mwaka 2013 ikiwa ina Tarafa 2, Kata 15, Vijiji 59 na Vitongoji 362. Halmashauri ya Wilaya ya Busega ina jumla ya Madiwani 20 ambapo madiwani 15 ni wa kuchaguliwa na Madiwani 5 ni wa viti maalum.

Kijiografia wilaya ya Busega inapakana na Wilaya ya Magu upande wa Magharibi, Wilaya ya Ukerewe upande wa kaskazini, Wilaya ya Bunda upande wa mashariki na kwa upande wa kusini imepakana na Wilaya ya Bariadi na Itilima. Wilaya ya Busega ina jumla ya ukubwa wa Kilometa za mraba 2129, ambapo Kilometa za mraba 1524 ni nchi kavu, na Kilometa za mraba 605 ni sehemu ya maji (Ziwa Viktoria).

LENGO LA JARIDA

Busega DC Jarida linalenga kuhabarisha na kuelezea shughuli za matukio mbalimbali makubwa ya Kiserikali Wilayani Busega, shughuli za utekelezaji wa Miradi na Matukio mengine muhimu Wilayani Busega. Pia Jarida hili linalenga kupanua wigo wa wakazi wa Busega na walio nje ya Busega kupata Habari na taarifa mbalimbali za shughuli za maendeleo zinazotekelezwa Wilayani humo. Jarida hili huandaliwa na Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Busega. Toleo la Jarida hili huchapishwa kila baada ya Miezi Mitatu. Pia kupata taarifa, matangazo na miongozo mbalimbali unaweza kutembelea Tovuti ya Halmashauri: www.busegadc.go.tz na Mitandao ya Kijamii Instagram: Busega_Dc; Facebook: Halmashauri ya Wilaya ya Busega na YouTube Channel: BusegaDc

www.busegadc.go.tz
@busegadc busegadc
@busegadistrict halmashauri ya wilaya ya busega

RAIS SAMIA AAHIDI UJENZI WA STENDI NA SOKO MJI WA LAMADI

Kutoka ***Lamadi-Busega***

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan amesema Serikali itajenga kituo cha mabasi na soko katika mji wa Lamadi Wilayani Busega. Samia ameyasema hayo wakati akiwa njiani kuelekea mkoani Mara tarehe 04/02/2022 ambako atakuwa na ziara ya siku nne.

Akiongea na wakazi hao wa Lamadi ambao walijitokeza asubuhi na mapema kwa wingi, Rais Samia amesema suala la stendi tumelichukua na Serikali itajenga kituo cha mabasi na soko. “Nimemsikia hapa Mkuu wa Mkoa amesema kiasi cha ujenzi wa stendi ni takribani TZS bilioni 1.6, kwa kiasi hicho cha fedha Serikali hainshindwi kujenga stendi, tutajenga hiyo stendi na soko hapa Lamadi” aliongeza Mhe. Samia.

Picha: **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akiwasilimia Wananchi wa Lamadi wilayani Busega, Simiyu wakati akielekea Mkoani Mara kikazi mwanzoni mwa mwezi wa kwanza mwaka huu.**

Aidha, Rais Samia ameiagiza Wizara ya Maliasili na Utalii kuhakikisha wanatatua kero za wananchi wa Lamadi ya kuvamiwa na wanyama ikiwemo tembo na viboko. “Pamoja na juhudi mnazoendelea kufanya lakini hakikisheni mnaweka kituo cha maliasili maeneo haya ili kupunguza adha ya wanyama hatarishi kwa wananchi”, alisema Rais Samia.

www.busegadc.go.tz
@busegadc busegadc
@busegadistrict halmashauri ya wilaya ya busega

Awali, Mkuu wa Mkoa wa Simiyu Mhe. David Kafulila ameweza kueleza juhudi kubwa ambazo Serikali ya awamu ya sita inazifanya katika mkoa wa Simiyu, ikiwemo uboreshwaji wa miundombinu ya barabara, shule na huduma za maji na kueleza baadhi ya kero na changamoto zinazowakabili wakazi wa Lamadi ikiwemo kutokuwepo kwa stendi na soko la uhakika ambavyo vimekuwa kero kwa wakazi hao. Kafulila amesema Simiyu imekuwa ikiendelea kwa kasi kutokana na juhudi za Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan. “Katika kipindi cha awamu ya sita mkoa wa Simiyu umepokea zaidi ya TZS bilioni 126 kwaajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo katika mkoa wa Simiyu, aliongeza Kafulila.

Kwa upande wake mbunge wa jimbo la Busega Simon Songe amemshukuru sana Mhe. Rais kwa kazi anayoendelea kuifanya kwani mpaka sasa mambo makubwa yamefanyika katika Wilaya ya Busega, hivyo anashukuru sana kwa maendeleo yanayoendelea kufanyika chini ya Serikali sikivu ya awamu ya sita.

Pichani: **Mkuu wa Wilaya ya Busega Mhe. Gabriel Zakaria akiwa na Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Busega Bi. Veronica Sayore wakifurahia jambo wakati wa mapokezi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mji wa Lamadi wakati Mhe. Samia Suluhu Hassan alipokuwa anapita kuelekea mkoani Mara kwa ziara ya kikazi mwezi Januari mwaka huu.**

“Tunashukuru sana kwa fedha nyingi ikiwemo fedha za ujenzi wa madarasa 95 ambayo yamesaidia upungufu wa madarasa katika jimbo la Busega, kwani watoto wote waliofaulu kujiunga kidato cha kwanza wameanza masomo kwa pamoja, sisi wananchi wa Busega hatusemi tu kwamba unaupiga mwingi bali unaupiga mwingi sana”, aliongeza Songe.

Pamoja na

www.busegadc.go.tz
@busegadc busegadc
@busegadistrict halmashauri ya wilaya ya busega

hayo, Mhe. Samia Suluhu Hassan amempongeza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashuri ya Wilaya ya Busega Veronica Sayore kwa kusimamia vyema ujenzi wa vyumba vya madarasa 95 yaliyojengwa chini ya mpango wa maendeleo kwa ustawi wa Taifa na mapambano dhidi ya UVIKO 19. “Kituo nilichotoka nimetengua wakurugenzi wanne kutokana na ubadhilifu na matumizi mabaya ya fedha, kwako sijasikia kwahiyo endelea kuchapa kazi Mkurugenzi” aliongeza Rais Samia.

Akiongelea suala la ufanyaji wa biashara ndogondogo, Rais Samia amewataka wafanyabiashara wadogo maeneo ya Lamadi na Sehemu nyinginezo kuwa wavumilivu kwani Serikali ina mpango mzuri juu yao ya kutenga maeneo ya kufanya shughuli zao za biashara. “Serikali ina mpango mzuri, tukifanikiwa Tanzania itakuwa na maeneo mengi ya kufanyia biashara kwa muda wa masaa ishirini na nne” alisema Rais Samia.

Rais Samia Suluhu Hassan anaeleka mkoani Mara kwa ziara ya siku nne, pamoja na mambo mengine atashiriki kilele cha maadhimisho ya miaka 45 ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ambayo kitaifa yanafanyika siku ya kesho tarehe 05/02/2022 mkoani humo.

www.busegadc.go.tz
@busegadc
busegadc
halmashauri ya wilaya ya busega

VIKUNDI 17 WILAYANI BUSEGA VYANUFAIKA NA MIKOPO YA ASILIMIA 10 YENYE THAMANI YA TZS MILIONI 132.54

Kutoka-Busega

Vikundi 17 vya wajasiriamali Wilayani Busega vimenufaika na mikopo ya asimilia 10 itokanayo na mapato ya ndani, ambapo kiasi cha TZS milioni 132.54 kimetolewa na Halmashauri ya Wilaya ya Busega kwa makundi ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Kati ya fedha hizo TZS milioni 86.325 kimetokana na mapato ya ndani ya bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022 ambayo sawa na asilimia 49.9 na kiasi cha TZS milioni 46.215 kimetokana na

Picha: Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega Bi. Veronica Sayore akiongea na vikundi (hawapo pichani) vilivyopewa mikopo ya asimilia 10 ya Halmashauri. Aliyekaa ni Afisa Maendeleo ya Jamii Wilaya ya Busega Bw. Dismas Ijagala.

www.busegadc.go.tz
@busegadc busegadc
@busegadistrict halmashauri ya wilaya ya busega

Akizungumza wakati alipokutana na vikundi hivyo, Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Busega, Veronica Sayore amesema

mikopo hiyo yenye masharti nafuu imetolewa ikiwa ni utekelezaji wa sheria ya utoaji mikopo

kwa wajasiriamali wa makundi ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Sayore amevitaka vikundi hivyo kuhakikisha wanazielekeza fedha hizo katika malengo yao waliyojiwekea kwa kila kikundi na sio vinginevyo. “Matumizi ya fedha hizi za mikopo zitumike katika malengo yale mliojiwekea ili kuhakikisha mnarejesha kwa wakati na sio vinginevyo” aliongeza Sayore.

Kwa upande mwingine Sayore amesema kumekuwa na vikundi ambavyo vinashindwa kurudisha fedha za mikopo kwa wakati hivyo hukwamisha shughuli za ukopeshaji kwa wahitaji wengine. “Tunaomba mrudishe mikopo hiyo kwa wakati, ili kusaidia wengine wenye uhitaji wa mikopo hiyo, wale ambao hawarudishi kwa wakati mnakwamisha, sitarajii kuliona hilo kutoka kwenu”, alisema Sayore.

Kwa upande wake Afisa Maendeleo ya Jamii Wilaya ya Busega, Dismas Ijagala amewaasa wanufaika kutumia mikopo hiyo kwa usahihi ili kuepusha sintofahamu wakati wa urejeshwaji wa mikopo hiyo. “Vipo baadhi ya vikundi ambavyo vimekuwa na upotevu wa fedha wanazokopeshwa, hii inasababishwa na kutokuwa na matumizi sahihi ya fedha hizo, alisema Ijagala.

Aidha, Sayore amesema hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi ya vikundi ambavyo vitaonesha kutorejesha fedha hizo kwa wakati. Halikadhalika, Sayore amesema kupitia mikopo hii ya asilimia 10 ya wajasiriamali itasaidia vikundi hivyo kuongeza mtaji wa shughuli zao za kiuchumi.

Pamoja na hayo, Sayore amevitaka vikundi hivyo kuimarisha umoja ili vikundi hivyo vidumu katika misingi ya kujenga uchumi wa mtu mmojammoja. Kwa upande wa wafaidika wameshukuru kwa mikopo hiyo na kuahidi kuitumia mikopo hiyo kulingana na malengo waliyojiwekea. Halmashauri ya Wilaya ya Busega imetoa kiasi cha fedha hiyo ikiwa ni mpaka kufikia robo ya pili ya mwaka wa fedha 2021/2022 ambapo vikundi 12 vya wanawake, vimepata kiasi cha TZS milioni 63.54, vikundi 4 vya vijana TZS milioni 57 na kikundi 1 cha watu wenye ulemavu TZS milioni 12.

www.busegadc.go.tz
@busegadc busegadc
@busegadistrict halmashauri ya wilaya ya busega

BARAZA LA MADIWANI LAPITISHA MAPNGO WA BAJETI WENYE ZAIDI YA TSH BILIONI 32.397 KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

Kutoka-Busega

Baraza la madiwani Halmashauri ya Wilaya ya Busega limepitisha bajeti ya jumla ya Tsh **32,397,778,860** kwaajili ya mwaka wa fedha 2022/2023. Baraza hilo ambalo limefanyika tarehe 23/02/2022, ambapo wajumbe wa baraza hilo wameridhishwa na vile bajeti hiyo ilivyotayarishwa.

Mwenyekiti Halmashauri ya Wilaya ya Busega Mhe. Sundi Muniwe amesema anaamini bajeti hiyo ambayo imepitishwa kwaajili ya utekelezaji wake kwa mwaka ujao wa fedha, itakidhi matakwa ya Halmashauri kwakuwa imekuwa bajeti iliyoelekezwa zaidi kwenye vipaumbele vya Halmashauri.

Picha: Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega Mhe. Sundi Muniwe akiongoza kikao cha Baraza la Madiwani kilichopitisha Bajeti ya Mwaka wa fedha 2022/2023. Wengine ni Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri Mhe. Ng'habi Mojo (aliyekaa Kushoto), Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Busega Bi. Veronica Sayore

"Tuna imani kubwa na bajeti hii kwa maana imeandaliwa vyema tofauti na baadhi ya bajeti za miaka iliyopita, hivyo ikitekelezwa katika uhalisia wake

www.busegadc.go.tz
@busegadc busegadc
@busegadistrict halmashauri ya wilaya ya busega

tutafikia malengo ya vipaumbele tulivyojiwekea", alioneza Muniwe.

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Busega, Veronica Sayore amesema kwamba utekelezaji wa bajeti unategemea na upatikanaji wa fedha, na anamini bila shaka bajeti iliyopitishwa na baraza la madiwani itasimamiwa vyema ili kutekeleza yale yote yaliyopendekezwa. "Tutasimamia vyema utekelezaji wa bajeti iliyopitisha, ili kuhakikisha vipaumbele vilivyobainishwa ikiweo miradi ya maendeleo inatekelezwa", alisema Sayore.

Aidha, Sayore amesema, miradi mbalimbali na vipaumbele vilivyobainishwa itatekelezwa kwa wakati kwa kusimamia vyema mapato ya ndani ili kutekekleza miradi mbalimbali inayotokana na fedha za mapato ya ndani. "Tutaimarisha vikosi kazi, na mbinu mpya zitakazoongeza mapato ya Halmashauri kwa kiasi kikubwa ili kuwezesha utekelezaji wa bajeti hii", aliongeza Sayore.

Madiwani wanasema bajeti hii ina maono mazuri kwani imeainisha maeneo muhimu ambayo yataleta chachu kubwa ya Maendeleo kwa Wilaya ya Busega. Miongoni mwa vipaumbele vilivyobainishwa ni pamoja na utengenezaji wa miundombinu katika taasisi zikiwemo shule, Zahanati na vituo vya afya. Maeneo mengine ni pamoja ya kuimarisha ustawi wa jamii kwa kutoa Mikopo ya asilimia 10 na kusimaia vyema fedha za mpango wa kunusuru kaya masikini (TASAF).

Bajeti ya Halmashauri ya Wilaya ya Busega kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imepitishwa na baraza la madiwani, ikiwa imetokana na vyanzo vitatu, ikiwemo ruzuku kutoka Serikali

kuu ikiwa ni Tsh 23,859,949,340 sawa na asilimia 73.6, fedha za wahisani Tsh 5,769,585,720 sawa na asilimia 17.8 na vyanzo vya mapato ya ndani Tsh 2,768,243,800 sawa na asilimi 8.5.

WAKULIMA ZAO LA PAMBA WAPEWA ELIMU YA UPULIZIAJI VIUATILIFU

Kutoka-Busega

Wakulima wa zao la Pamba Wilayani Busega wameanza kupatiwa elimu ya upuliziaji dawa katika mashamba yao ili kuondoa wadudu waharibifu wa zao hilo. Katika mafunzo hayo ya siku tatu kuanzia tarehe 07-09 Machi, 2022 yanajumuisha wakulima wa zao hilo katika Kata zote 15 zilizopo Wilayani Busega.

Picha: Mkuu wa Wilaya ya Busega Mhe. Gabriel Zakaraia (wa kwanza kushoto), Balozi wa zao la Pamba nchini Bw. Aggrey Mwanri (wa pili kutoka kushoto) wakiwa kijiji cha Nyamatembe na Wakulima wa zao la Pamba, ambapo elimu ya upuliziaji viuatilifu ilitolewa.

Balozi wa zao la Pamba nchini Bw. Aggrey Mwanri akiambata na mwenyeji wake Mkuu wa Wilaya ya Busega Mhe. Gabriel Zakaria wameweza kukutana na wakulima katika maeneo yao ili kutoa elimu ya moja kwa moja kwa vitendo. Katika Mafunzo hayo wakulima wanaelimishwa namna bora ya uchanganyaji wa dawa na upuliziaji unaostahili ili kudhibiti wadudu waharibifu.

www.busegadc.go.tz
@busegadc busegadc
@busegadistrict halmashauri ya wilaya ya busega

"Lengo la kuja kukutana na wakulima katika mashamba yao ni kuonesha namna ya uchanganyaji na upuliziaji wa dawa katika shamba ili kudhibiti wadudu waharibifu wakiwemo funza na chawa jani", alisema Mwanri. Aidha, Mwanri

amesema ili kuwa na tija ya zao la Pamba ni vyema wakulima kupatiwa elimu ya mara kwa mara ya jinsi ya uchanganyaji wa dawa na upuliziaji kwani juhudi za wakulima zitarudishwa nyuma pale tu udhibiti wa wadudu utapuuziwa.

Mkuu wa Wilaya ya Busega Mhe. Gabriel Zakaria amewataka wakulima kufuata maelekezo ya wataalam ili kuwa na uzalishaji wenye tija wa zao hilo kuliko kulima kwa mazoea kama ilivyo hapo awali. "Tujiatahidi kufuata maelekezo ya wataam ili kuongeza uzalishaji wa Pamba na kufikia lengo la Wilaya la kuzaliza tani 50,000 kwa msimu wa mwaka huu, tulime kwa kufuata vipimo vya wataalam kama ilivyoelekezwa kwamba ni umbali wa sentimeta 60-30 kutoka shina moja hadi lingine, alisema Zakaria.

Pamoja na hayo, Zakaria ameweza kuwapatia mabomba ya kupulizia dawa wakulima ambao wamefanya vizuri zaidi kwa lengo la kuwaongezea motisha zaidi, huku akitoa tahadhari kwa wote ambao watagawa dawa hizo bila kuzangatia miongozo na taratibu. Nao wakulima wa Pamba wameishukuru Serikali ya Awamu ya Sita na kumshukuru Rais wa jamhuri ya muungano wa Tanzania mhe. Samia suluhu Hassan kwa hatua anazoendelea kuzifanya ikiwemo utoaji wa mkopo wa viuatilifu kwa wakulima kwa lengo la kuhakikisha wakulima wanapata uzalishaji wenye tija kubwa.

www.busegadc.go.tz
@busegadc busegadc
@busegadistrict halmashauri ya wilaya ya busega

Picha: Naibu Katibu Mkuu wa CCM Taifa kwa upande wa Tanzania Bara Ndg. Christine Mndeme (wa pili kutoka kulia), akiwa na viongozi wa Wilaya ya Busega. Ndg. Mndeme alitembelea kukagua mradi wa ujenzi wa kituo cha afya Mkula.

SEKRETARIETI YA HALMASHAURI KUU YA CCM TAIFA YARIDHISHWA NA USIMAMIZI WA UJENZI WA MIRADI YA MAENDELEO WILAYANI BUSEGA

Kutoka-Busega

Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya Chama cha Mapinduzi Taifa (CCM) ikiongozwa na Katibu Mkuu wa Chama hicho Ndg. Daniel Chongolo imefanya ziara ya siku mbili wilayani Busega tarehe 31/01/2022 hadi 01/02/2022 kwa lengo la kukagua miradi ya maendeleo, na kuangalia shughuli mbalimbali zinazoendelea Wilayani Busega na kuridhishwa na utekelezaji wa miradi hiyo.

Katika siku ya kwanza ya ziara hiyo Wilayani Busega Naibu Makatibu wa

www.busegadc.go.tz
@busegadc busegadc
@busegadistrict halmashauri ya wilaya ya busega

CCM Taifa kwa upande wa Tanzania Bara na Zanzibar Ndg. Christine Mndeme na Ndg. Dkt. Abdalah Mabodi wakimwakilisha Katibu Mkuu walitembelea kukagua mradi wa ujenzi wa kituo cha Afya Mkula na mradi wa vyumba vya madarasa 14 katika shule ya Sekondari Kabita, madarasa yaliyojengwa chini ya mpango wa maendeleo kwa ustawi wa Taifa na mapambano dhidi ya UVIKO-19.

Mradi wa ujenzi wa kituo cha Afya Mkula ambao ujenzi wake unagharimu kiasi cha TZS milioni 400 na ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje (OPD), jengo la upasuaji na jengo la wodi ya wazazi na ujenzi wa majengo hayo unaendelea. Ukamilikaji wa ujenzi wa kituo hicho utahudhumia zaidi ya wananchi 16,800 wa Kata hiyo na wananchi wa maeneo ya karibu. Ujumbe wa Sekretarieti hiyo umeelekeza kwamba huduma zianze tu pale majengo muhimu yatakapokamilika. “Tungependa kuona majengo haya yaanze kutumika tarehe 28/02/2022 kwa majengo yaliyokamilika mkiendelea kumalizia majengo yaliyobaki ili wananchi wa Mkula waweze kupata huduma” aliongeza Mndeme.

Aidha, Naibu Katibu CCM Taifa upande wa Bara Ndg. Christine Mndeme amewaasa wananchi wa Kata hiyo na Busega kwa ujumla kutumia huduma za hospitali ili kuokoa maisha yao hasa wakina mama. “Tunapaswa kushawishi na kutoa elimu kwa wanachi hasa wajawazito kuja kuhudhuria kliniki na kujifungulia katika vituo vya Afya ili kuokoa maisha ya mama na mtoto” alisema Mndeme.

Halikadhalika, ziara hiyo ilitembelea mradi vyumba vya madarasa yaliyojengwa chini ya mpango wa maendeleo kwa ustawi wa Taifa na mapambano dhidi ya UVIKO-19 katika shule ya Sekondari Kabita ambapo jumla ya TZS milioni 280 imetumika kujenga vyumba 14 vya madarasa. Sekretarieti hiyo imeridhika na ujenzi wa vyumba hivyo vya madarasa ambavyo vimeanza kutumika. Aidha, Mndeme amesema changamoto za vyumba vya madarasa kwa shule za msingi ni jambo ambalo wao kama chama wanaendelea na mikakati ili Serikali iweze kutatua tatizo hilo kama ilivyo kwa shule za sekondari. Kwa upande mwingine ujumbe wa Sekretarieti hiyo imeagiza Halmashauri ya Wilaya ya Busega kuona namna ya kujenga miundombinu katika shule ya msingi Masangani ambayo kwasasa ni shule shikizi.

Katika siku ya pili ya ziara hiyo ujumbe wa Sekretarieti CCM Taifa ilifanya ziara ya kukagua ujenzi wa wodi tatu katika hospitali ya Wilaya ya Busega, ambapo Serikali imetoa kiasi cha TZS milioni 500 kwaajili ya ujenzi wa wodi ya wanaume, wanawake na watoto. Ujumbe wa Sekretarieti ya CCM Taifa iliridhika na mwenendo wa ujenzi wa wodi hizo na kusisitiza kwamba huduma za Afya ziendelee kutolewa kwa ufanisi mkubwa kwani lengo la Serikali ni kufikisha huduma bora kwa wananchi ikiwemo huduma za Afya.

Ujumbe wa Sekretarieti hiyo umeagiza kuharakisha utengenezwaji na uwekaji wa miundombinu ya maji, barabara na umeme katika hospitali ya Wilaya na vituo vya Afya ili kuwezesha huduma bora za Afya. Pamoja na mengineyo, ujumbe wa Sekretarieti hiyo ulipata

muda wa kukutana na kuzungumza na baraza la wazee wa Busega ili kusikiliza kero na changamoto zao zinazowakali na kutembelea mashina ya chama hicho.

Uongozi wa Wilaya ya Busega ukiongozwa na Mkuu wa Wilaya ya Busega Mhe. Gabriel Zakaria imetoa shukrani kubwa kwa Sekretarieti ya CCM Taifa. “Tutafanyia kazi yote yaliyoelekezwa ili kuondoa changamoto zilizopo” aliongeza Zakaria.

JUMLA YA TZS 2,245,850,000 KUJENGA BARABARA ZA VIJIJINI WILAYANI BUSEGA

Kutoka-Busega

Zaidi ya Bilioni 2.245 zinatarajia kutumika kujenga barabara za vijijini Wilayani Busega. Hayo yamesemwa na

Picha: Mkuu wa Wilaya ya Busega Mhe. Gabriel Zakaria akiwa katika kikao cha wadau wa barabra Wilaya ya Busega.

www.busegadc.go.tz
@busegadc busegadc
@busegadistrict halmashauri ya wilaya ya busega

Meneja wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) Mhandisi Mwita Muhochi katika kikao kilichofanyika siku ya tarehe 24/01/2022 kwaajili ya kupitia utekelezaji wa miradi ya barabara kwa mwaka 2021/2022 na kupitia mapendekezo ya mpango wa mwaka 2022/2023 kwa wadau wa barabara.

Katika kikao hicho, Mhandisi Muhochi amesema kwamba Serikali imeleta kiasi hicho ili kuhakikisha barabara za vijijini zinajengwa kwa

ubora ili kuondoa changamoto za miundombinu ya barabara Wilayani Busega.

Mkuu wa Wilaya ya Busega Mhe. Gabriel Zakaria amesema Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Mhe. Samia Suluhu Hassan ina malengo makubwa ya kuhakikisha barabara zinajengwa maeneo mbalimbali kwa ubora unaotakiwa. Aidha, Zakaria amesme licha ya Serikali kuleta fedha hizo ni vyema watekelezaji kuwa na usimamizi mzuri ili ziweze kutumika kwa ufanisi mkubwa. “Niwapongeze TARURA kwa kazi nzuri mnayoendelea kuifanya lakini ni muhimu Wakandarasi tunaowapa kazi wawe na uwezo wa kufanya kazi, kwani baadhi wamekuwa na shida ya kutokamilisha miradi ya ujenzi wa barabara kwa wakati” alisema Zakaria.

Kutowapa nafasi Wakandarasi wanaochelewesha kazi ni miongoni mwa mambo yaliyo jadiliwa kwa kina katika kikao hicho, huku wadau mbalimbali wakikiri kwamba kuna baadhi ya wakandarasi wamekuwa wakicheleweshaujenzi wa miradi ya barabara hivyo kusababisha adha kwa wananchi wa maeneo husika.

Aidha, Zakaria amewataka TARURA kushirikiana na madiwani katika miradi ya ujenzi wa barabara ili kuleta tija ya utekelezaji wa miradi hiyo katika maeneo husika. “Madiwani wakishirikishwa ipasavyo itasaidia kuleta tija na vipaumbele katika maeneo husika”, aliongeza Zakaria.

Wadau walioshiriki kikao hicho wanasema kwamba kazi kubwa imefanywa na TARURA kwani kwasasa sehemu kubwa ya Wilaya inafikika ukilinganisha na hapo awali. Aidha, wameomba barabara ambazo bado hazijasajiliwa kwenye mtandao wa barabara zisajiliwe ili ziweze kufunguliwa, na barabara zote ambazo zina umuhimu mkubwa kwa uchumi wa wananchi kupewa kipaumbele katika matengenezo. Nae Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega Mhe. Sundi Muniwe amesema kwamba madiwani wataendelea kushirikiana na TARURA ili kuhakikisha barabara zinajengwa kwa ufanisi mkubwa.

Mtandao wa barabara Wilayani Busega ni kilomita 511 huku kilometa 159.73 sawa na asilimia 31 zipo katika hali nzuri, kilometa 124.01 sawa na asilimia 25 zipo katika hali ya wastani na kilometa 227.36 sawa na asilimia 44 bado zipo katika matengenezo ya awali, wakati asilimia 35 ya barabara zilizotengenezwa zipo katika kiwango cha changarawe (moram) na asilimia 65 ni barabara za udongo. TARURA Wilaya ya Busega inatarajia kutengeneza barabara zipatazo 30 zenye urefu wa zaidi ya kilometa 68.

www.busegadc.go.tz
@busegadc busegadc
@busegadistrict halmashauri ya wilaya ya busega

WATUMISHI WATAKIWA KUSHIRIKI MICHEZO ILI KUIMARISHA AFYA

Kutoka Nyashimo-Busega

Watumishi wa Umma Wilayani Busega wametakiwa mara kwa mara kushiriki katika michezo ili kujenga na kuimarisha afya zao. Hayo yamesemwa na Mkuu wa Wilaya ya Busega Mhe. Gabriel Zakaria wakati wa bonanza la michezo lililofanyika siku ya Jumamosi 19 Machi 2022, ambapo limeshirikisha taasisi za Serikali zilizopo Wilayani Busega.

Zakaria amesema ni vyema Watumishi wakashiriki michezo ili kuimarisha afya, kwani ushiriki katika michezo kwa kiasi kikubwa humfanya mtu kutokuwa na magonjwa ambayo hudhoofisha afya. “

Picha: Mgeni rasmi ambae ni Mkuu wa Wilaya ya Busega Mhe. Gabriel Zakaria (wa kwanza kushoto) akikagua kikosi cha timu ya mpira wa miguu ya Halmashauri ya Wilaya ya Busega wakati wa Bonanza la taasisi za Serikali zilizopo Wilayani Busega.

Bado mwamko ni mdogo wa ushiriki katika michezo, nimekuwa nikishiriki

www.busegadc.go.tz
@busegadc busegadc
@busegadistrict halmashauri ya wilaya ya busega

mazoezi, lakini wanaohudhuria ni wachache sana na wengi wakiwa ni wanafunzi, naomba tushiriki katika michezo kwa wingi ili kuimarisha afya zetu". Aliongeza Zakaria. Kwa upande mwingine Zakaria amesema kupitia michezo mbalimbali ikiwemo ya dansi, vijana wengi wanaweza kujiajiri na kujipatia kipato kikubwa kama ilivyo kwa baadhi ya wasanii wakubwa waliopo nchini. "Mimi ni mdau mzuri wa michezo, na nipo tayari kuwa mstari wa mbele kuhakikisha tunakuwa na michezo mbalimbali Wilayani kwetu ili kutengeneza ajira kwa vijana wetu, kwani licha ya michezo kusaidia kuimarisha afya lakini pia hutengeneza ajira", alisema Zakaria.

Washindi wa michezo mbalimbali walipatiwa zawadi ambapo kwa upande wa mpira wa miguu wanaume, timu ya Polisi Busega ilifanikiwa kuwa mshindi wa kwanza baada ya kuifunga timu ya Halmashauri Makao Makuu katika mchezo wa fainali kwa mikwaju ya penati 5-4, upande wa netiboli timu ya walimu iliibuka kidedea baada ya kuifunga timu ya Halmashauri Makao Makuu. Kwa upande wa riadha wanaume mita 100 mshindi ni Mohamed Rashid ambaye ni Mwalimu, mita 100 wanawake mshindi ni Piencia Mgizi ambae pia ni Mwalimu. Washindi wa nafasi ya kwanza hadi nafasi ya tatu kwa upande wa riadha na kukimbia kinyumenyume wamepatiwa fedha taslimu.Kwa mchezo wa kukimbia kinyumenyume mita 100 upande wa wanaume mshindi ni Betram Mwanga ambae ni Polisi, upande wa wanawake mshindi ni Piencia Mgizi ambae ni Mwalimu. Bonanza hilo linafanyika ikiwa na lengo la kuwaleta pamoja Watumishi wa Umma kwaajili ya kubadilishana mawazo, uzoefu na ujuzi mbalimbali.

Taasisi zilizoshiriki ni pamoja na timu ya Watumishi wa Halmashauri Makao Makuu Walimu Msingi, Walimu Sekondari, Watumishi Idara ya Afya, huku taasisi zinginezo zilizoshiriki ni TANESCO na Polisi, huku kila timu ikipata zawadi ya kondoo mmoja na pesa taslimu kwa mshindi wa kwanza na wa pili kwa upande wa mpira wa miguu. Washiriki wanasema kufanyika kwa bonanza hilo ni jambo jema na la Msingi, lakini wameomba viongozi na wadau kuwezesha bonanza hilo ili kuwa na ubora zaidi.